JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUSHIRIKI KATIKA KIKUNDI KAZI CHA (ITU) KUHUSU AKILI UNDE KWA MIJI NA JAMII ZA KISASA NA ENDELEVU

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina utaarifu Umma kuwa Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU) unawaalika watalaamu kushiriki katika Kikundi Kazi kipya kilichoanzishwa kuhusu Akili Unde kwa Miji na Jamii za Kisasa na Endelevu (FG-A14SSC).

FG-A14SSC ni jukwaa la kimataifa lililo wazi kwa ajili ya ushirikiano baina ya wataalamu kutoka ITU, mashirika mengine ya viwango, miji, sekta binafsi, taasisi za elimu, serikali, taasisi za Umoja wa Mataifa na wadau wengine husika. Kikundi Kazi hiki kimeanzishwa kwa kutambua nafasi inayozidi kukua ya Akili Unde katika upangaji, uendeshaji na uunganishaji wa miji na jamii. Kupitia kazi zake za awali kabla ya uandaaji wa viwango, Kikundi Kazi kitasaidia kubadilisha bunifu kuwa mifumo inayoweza kuingiliana, kukuzwa, kujumuisha makundi mbalimbali na kuwa endelevu, huku kikiweka msingi wa uandaaji wa viwango vya kimataifa katika siku zijazo.

Wito huu uko wazi kwa wataalamu wa mipango na uendeshaji wa miji, wahandisi, watafiti, wabunifu, wasimamizi wa sekta na wataalamu wa viwango ambao kazi zao zinahusiana na mifumo na huduma za mijini zinazotumia Akili Unde, miji na jamii za kisasa na endelevu, Mtandao wa Vitu (IoT), mifumo pacha ya kidijitali (digital twins) au utekelezaji wa mifumo katika ngazi ya miji. Ushiriki pia unahimizwa kwa wataalamu wanaowakilisha miji, serikali, sekta binafsi, taasisi za elimu, taasisi za utafiti, mashirika ya kuandaa viwango, taasisi za Umoja wa Mataifa, mashirika ya kimataifa na kikanda, asasi za kiraia pamoja na wadau wengine husika. Wataalamu wenye nia wanaalikwa pia kushiriki katika **Jukwaa la Akili Unde na Citiverse** litakalofanyika **tarehe 9 hadi 10 Septemba 2026,** pamoja na **mkutano wa kwanza wa FG-AI4SSC** utakaofanyika **tarehe 10 hadi 11 Septemba 2026, jijini Tampere, Finland.**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz

Kwa ajili ya kuonesha nia ya kutoa mchango, tafadhali tembelea kiungo kifuatacho: https://docs.google.com/forms/d/e/1FAIpQLSeywsgV6OTA37Y8Fkv3UxLTjChCgdxy4xF4oRGiKwf2revuEA/viewform.

Maelezo zaidi kuhusu Kikundi Kazi na mikutano iliyopangwa zinapatikana kupitia: https://www.itu.int/en/ITU-T/focusgroups/ai4ssc/Pages/default.aspx.

TCRA inawahimiza watalaamu wote wenye sifa kujisajili, kushiriki na kuwasilisha michango yao kabla ya tarehe ya mwisho wa kuwasilisha michango kwaajili ya mkutano wa kwanza.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni **tarehe 28 Agosti 2026.**

Imetolewa tarehe **15 Agosti, 2026**

Digitally Signed By
PETER PHILLIP MWASALYANDA
Sat Aug 15 15:03:48 EAT 2026

Mhandisi Peter P. Mwasalyanda
**MKURUGENZI MKUU**

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD